

USHAIRI: UTUNZI, UCHAMBUZI NA UWASILISHAJI

Kithaka a Mberia

Utangulizi

Katika mhadhara huu nitazungumza kuhusu “Ushairi: Utunzi, Uchambuzi na Uwasilishaji”. Labda tuanze kwa kujiuliza: Je, ushairi ni nini? Hili si swali rahisi kujibu. Ushairi ni utanzu wa fasihi, tanzu nyingine muhimu za fasihi zikiwa ni riwaya na tamthilia (au michezo ya kuigiza). Tanzu zote hizi hutumia lugha. Miogoni mwa sifa ambazo hutofautisha lugha ya ushairi na lugha ya tanzu nyingine za fasihi ni uchache na uzito wa maneno. Lugha ya ushairi huwa imechujwa. Maneno yake huwa yameteuliwa kwa makini. Pia mashairi huwa na muziki. Muziki huu hutokana na mdundo unaojengwa kwa kutumia njia mbalimbali.

Utunzi

Jambo la kwanza katika hatua za utunzi ni ilhamu. Ilhamu ni mvuto wa ndani kwa ndani unaoelekeza msanii (artist) kutunga kazi ya kisanaa. Kwa mfano, mvuto huu unaweza kutokana na jambo ambalo limemkumba msanii mwenyewe, kisa ambacho amekisikia au tukio ambalo ameshuhudia. Kama ilivyo kwa wasanii wengine, mshairi anaweza kupata ilhamu kutokana na jambo ambalo watu wengine hawalitili maanani. Hii hali ya msanii hutokana na mazoea yake ya kuiliza “KWA NINI?” katika akili yake kunapokuwa na jambo. Jinsi mshairi anavyojizoeza kuchunguza mambo katika akili yake ndivyo kutakapokuwa na uwezekano wa kupata ilhamu kutokana na mambo mengi.

Kuna wakati ambapo mshairi hutunga shairi mara tu baada ya kupata ilhamu. Wakati mwingine, mshairi husubiri mpaka ilhamu iimarike na kuiva vizuri ndani mwake kabla ya kutunga shairi.

Ili kuweza kutunga mashairi, tunahitaji kujua mbinu za utunzi. Mbinu hizo ni nyingi. Nitaelezea baadhi tu.

Miongoni mwa mbinu zinazotumiwa sana katika ushairi ni ile ijulikanayo kama JAZANDA. Jazanda ni ulinganishi wa kitu au jambo analolizungumzia mshairi na kitu au jambo jingine. Vitu hivyo viwili ni sharti vifanane angalu kwa baadhi ya sifa. Sifa inayolingana baina ya vitu hivyo viwili ndiyo mshairi huwa amedhamiria katika ujumbe wake. Tukisema “Onyango ni simba” au “Onyango, simba wa kijiji” tukinuia kumaanisha kwamba Onyango ana nguvu sana au ana ujasiri mwingi, tutakuwa tumetumia jazanda.

Kama ilivyo jazanda, tashibibi ni ulinganishi wa kitu kinachozungumziwa na mshairi na kitu kingine kinachofanana nacho. Hapa tena ni sharti vitu vinavyolinguishwa vishabihiane angalau kwa baadhi ya sifa. Ulinganishi wa kitashibibi unatofautiana na ule wa kijazanda kwa kuwa unatumia msamiati wa ulinganishi kama vile “kama”, “ja”, “mithili” na “mfano”. “Onyango ni kama simba” au “Onyango ana nguvu kama simba” ni tashibibi na wala sio jazanda.

Mbinu nyingine ya utunzi ambayo hutumiwa sana na washairi ni ile ijulikanayo kama TASHIHISI. Tashihisi ni matumizi ya lugha ambapo kitu hupewa uhai na hisia kinyume na hali yake halisi duniani. Katika kilele cha shairi lake zuri sana liitwalo “Usiniupe”, A. Abdalla anasema:

Uhai! Nakuliliya, wewe ndiye upendwaye
Uhai! Huna ubaya, yupi akutukiyaye?
A! Uhai niombeya, mamaangu sema naye
Pengine atasikiya, asiniupe mamangu.

Katika ubeti huo mshairi anazungumza na uhai. Uhai umepewa sifa za kibinadamu.

Wakati mwingine washairi hutumia MAFUMBO katika mashairi yao. Wanaeleza jambo kwa kuzungumzia jambo jingine tofauti kabisa. Kwa mfano, mshairi anaweza kuelezea maovu ya wanyonyaji kwa kuzungumzia wadudu wanyonya damu kama vile mbungo, chawa, kunguni, viroboto na mbu. Mshairi anaweza kuonyesha maangamizi ya dhalimu kwa kuelezea kishairi kuangamia kwa mnyama mkali kama vile simba, mbogo, kifaru au mamba. Mafumbo huwatumikia washairi katika vipengele mbalimbali vya ushairi. Kwa mfano, katika ushairi wa kimapenzi, mtunzi anaweza kutumia fumbo au mafumbo kuelezea mambo ambayo huwa ni mwiko kuzungumziwa kwa lugha ya moja kwa moja. Kwa kutumia fumbo au mafumbo mshairi atatimiza malengo yake bila kuhesabiwa kwamba ametumia lugha chafu.

Mbinu nyingine ambayo hutumiwa na washairi ni ile ya TASWIRA. Taswira ni picha inayochorwa na mshairi katika akili ya msomaji au msikilizaji wa shairi. Picha hiyo husawiriwa kwa kutumia lugha.

Wakati mwinginge washairi huelezea mambo kwa namna inayoyapa mambo hayo sifa zilizovuka kingo za uhalisia. Wanapofanya hivyo huwa wametumia mbinu ya CHUKU. Katika shairi la ‘Imani ya Mwana’, S. A. Mohamed anakipa kilio wingi wa machozi hivi kwamba machozi hayo yanajaza kikombe!

Si jambo lisilo la kawaida mshairi kuuliza swali huku tayari akijua jawabu lake. Maswali ya namna hiyo hayanuiwi kutafuta habari kama yalivyo maswali mengine katika lugha bali hudhamiriwa kutilia mkazo ujumbe anaouwasilisha mshairi. Hiyo ndiyo mbinu ya utunzi ijulikanayo kama BALACHA.

Wakati mwingine, katika kuelezea habari fulani, mshairi hutoa nafasi kwa mtu au kitu kinachohusika na habari hizo kuzungumza chenyewe. Mashairi anapofanya hivyo, yaani, anapoyanukuu maneno halisi yaliyosemwa, huwa anatumia mbinu ya utunzi iitwayo LITIFATI. Ubeti ufuatao unaonyesha matumizi ya litifati:

Alizoazoa nia
Akaturisha kifua
Akakaza misuli
Na kwa sauti ya chuma
Akakemea mauti
Ngo! Siendi!
Siendi kaburini!

Mshairi anaweza kutumia MLIO-ISHARA. Lugha zina milio ambayo hufanana au huwakilisha mambo, vitu na hali mbalimbali ulimwenguni. Milio hiyo huwa kama ishara ya kile kinachoshabihishwa nayo. Kwa mfano, ng'ombe hulia “ngo-o! ngo-o!”, miguu ya watu wanaokimbia hulia “kum! kum!”, ngoma ya msondo hulia “tum! tum!”, nao baadhi ya ndege huruka “bru! bru!” kutoka utanzu mmoja wa mti hadi utanzu mwengine. Mshairi anaweza kutumia milio kama hiyo kwa minajili ya kuyaimarisha maelezo ya kile ambacho husimamiwa na mliono.

Mbinu hizi na nyingine nyingi ndizo zinazoipa lugha ya ushairi uzito. Pia ndizo zinazomwezesha mshairi kutumia maneno machache katika kazi yake.

Kama tulivyotangulia kusema, mashairi huwa na mdundo. Mdundo huo unaweza kutokana na vina, mizani, na mikarara. Kupata vina na mizani katika shairi si jambo gumu ikiwa mshairi anajua njia zinazotumiwa kufikia lengo hilo.

Namna mojawapo ya kupata vina na mizani katika shairi ni kutumia mbinu za INKISARI, MAZIDA na TABDILA. Inkisari inatumika kupunguza mizani. Kwa mfano, tunaweza kulifupisha neno “usikate” na kulifanya “sikate”. Pia, tunaweza kutumia “babake” au “babaye” badala ya “baba yake”. Kutumia mazida kunaongeza mizani au, wakati nyingine, kutupatia kina tunachohitaji. Tunaweza kulibadili neno ‘mwili’ na kulifanya “muwili”. Tukifanya hivyo, tunapata mizani zaidi katika mstari. Pia tunaweza kubadili neno “kilio” na kulifanya “kiliyo”. Kufanya hivyo hakutaongeza mizani lakini kutatuwezesha kupata kina “yo” ikiwa tukihitaji. Tabdila inatumika kubadili sauti ili kupata kina. Kwa mfano, tunaweza kutumia “i” badala “a” mwishoni mwa neno “maana” ili tupate “maani” badala ya “maana”. Kufanya hivyo tutatuwezesha kupata kina “ni” endapo tunakihitaji.

Uchambuzi

Ili kuweza kuchambua mashairi vizuri, tunapaswa kuelewa namna mbinu za utunzi zinavyotumiwa. Bila kuelewa namna mbinu hizi zinavyotumiwa, itakuwa vigumu kufasiri matumizi yake katika shairi. Pia itakuwa vigumu kufafanua mambo mbalimbali tunapozungumza kuhusu shairi. Kwa hivyo, ili kufikia uchambuzi mzuri wa mashairi, hatuna budi kujifunza mbinu mbalimbali za utunzi.

Tukitaka kulichambua shairi inatubidi kulisoma kwa makini na kwa mara kadhaa. Wakati wa kulisoma ni muhimu kutilia maanani siyo tu maneno yake bali pia muundo na uakifishi (punctuation) wake. Uakifishi ni muhimu sana katika shairi. Mambo kama vile vituo, vikomo, matumizi ya herufi ndogo au kubwa hayana budi kuzingatiwa kwa makini.

Jambo jingine muhimu katika uchambuzi wa mashairi ni muktadha wa shairi. Kuna manufaa kutokana na kujua mahali na wakati shairi lilipotungwa. Pia kuwa na habari kuhusu mtunzi ni jambo linalomfaidi mchambuzi. Hata hivyo, mambo haya si ya lazima.

Tunaposoma shairi na kugundua kwamba hatuelewi kinachozungumziwa, tusikate tamaa. Tulusome tena na tena. Tunapogundua kwamba kuna sehemu ambayo tunaielewa kuliko sehemu nyingine, tuisome sehemu hiyo kwa makini zaidi. Baada ya kuielewa vizuri, tujaribu kuitumia kufasiri sehemu nyingine za shairi.

Uwasilishaji:

Kuna njia mbalimbali za kuwasilisha mashairi. Tunaweza kuwasilisha kwa kutumia sauti ya binadamu pekee. Pia tunaweza kuyawasilisha kwa kutumia sauti ya binadamu ikiandamana na muziki wa ala za muziki.

Shairi laweza kuwasilishwa na mtu mmoja, watu wawili au zaidi. Laweza kuwasilishwa kwa kulikariri, kuliimba, kuliigiza au kulisoma.

Tunapowasilisha mashairi, ni muhimu kuzingatia maudhui na ujumbe wa shairi. Ili kufaulu kuwasilisha ujumbe ulionuiwa na mshari, hatuna budi kutilia maanani mambo kadha wa kadha. Mambo haya ni pamoja na matumizi mazuri ya vipengele mbalimbali vyta sauti, kutumia ishara za uso na mikono kwa namna inayofaa na pia kutumia vizuri nafasi jukwaani.

Njia za uwasilishaji ambazo tumetaja zinahusu uwasilishaji wa mashairi kwa jumla. Baadhi ya njia hizo haziruhusiwi kwenye Tamasha za Muziki za Kenya (Kenya Music Festival). Kwa hivyo, ni muhimu muwasilishaji wa shairi katika tamasha hizo kuelewa vizuri njia zinazokubalika na waandalizi wa tamasha.

Hitimisho:

Ningependa kumalizia mhadhara huu kwa kutoa mfano wa shairi langu liitwalo “Wimbo wa - Amba”. Katika shairi hili “Amba” imeradidiwa ili kujenga mdundo katika shairi.

Wimbo wa “-Amba”

Nitaimbia “-AMBA”
Hivi kwamba
Nimalizapo kuamba
Nitakuwa nimeamba
Juu yake mamba
Mwenye kujigamba
Na wacheleao kuamba
Katika shamba

Natangaza kwamba

Huyu mamba
Ndiye mwamba
Unaoharibu shamba

Naamini kwamba
Ingawa amejipamba
Kwa magamba
Hatashinda kamba
Ivunjayo miamba
Kwenye mashamba

Nilishuhudia mamba
Ambaye akijigamba
Kutochelea wanashamba

Hakushinda kamba
Ya wanashamba
Walipoanza kuamba
Katika shamba

Ukiniona muamba
Apendaye kuamba
Nitajibu kwamba
Sipendi kuamba
Bali mamba
Mwenye kujigamba
Na wanashamba
Wacheleao kuamba
Wamenifanya kuamba

Nahitimisha ‘-amba’
Kwa kukariri kwamba
Ivutwapo kamba
Ya wanashamba
Waanzapo kuamba
Jahili mamba
Hatakosa kuamba:
Nilikosea kujigamba
Nikinena kwamba
Mimi mamba
Tayari nimejipamba
Kwa magamba
Kunyamazisha wasioamba
Katika shamba
Wamuapo kuamba.

Mhadhara huu ultolewa katika warsha mojawapo ya zile zilizoandaliwa na Tamasha za Muziki za Kenya (Kenya Music Festival) za Wizara ya Elimu nchini Kenya. Warsha hizo zililengwa kuwapa walimu wa shule na vyuo maarifa na stadi za kuwawezesha kuwaanda vizuri wanafunzi wao ili washiriki na kushindana katika tamasha ambazo, ingawaje shughuli yake kubwa ilikuwakuhusu muziki, zilijumuisha pia ukariri wa mashairi na uzungumzaji.